IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

N05/2/ABSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

88052391

**SWAHILI B – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI B – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI B – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Thursday 3 November 2005 (morning)
Jeudi 3 novembre 2005 (matin)
Jueves 3 de noviembre de 2005 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N'ouvrez pas ce livret avant d'y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l'épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

OFA ZOTE ZINAKUJA NA:
- ✔ UJUMBE WA SAUTI WA **BURE**
- ✔ HUDUMA YA NIPIGIE **BURE**
- ✔ HUDUMA YA KUTUMA CREDIT **BURE**
- ✔ HUDUMA KWA MTEJA MASAA 24 **BURE**

# TUNA NJIA SITA ZAIDI ZA KUKUFANYA UWE WA KWANZA

## NJIA 6 ZAIDI ZA KUFAIDIKA KUTOKA VODASHOP



| NOKIA 2100 | NOKIA 5110 | NOKIA 1100 | MOTOROLA C200 | SAMSUNG R220 | NOKIA 6110 |
|---|---|---|---|---|---|
| ILIYOUNGANISHWA PAMOJA NA | ILIYOUNGANISHWA PAMOJA NA | ILIYOUNGANISHWA PAMOJA NA | ILIYOUNGANISHWA PAMOJA NA | ILIYOUNGANISHWA PAMOJA NA | ILIYOUNGANISHWA PAMOJA NA |
| TSH. 1000/- ZA MUDA WA MAONGEZI | TSH. 1000/- ZA MUDA WA MAONGEZI | TSH. 1000/- ZA MUDA WA MAONGEZI | TSH. 1000/- ZA MUDA WA MAONGEZI | TSH. 1000/- ZA MUDA WA MAONGEZI | TSH. 1000/- ZA MUDA WA MAONGEZI |
| TSH. 111,999/- | TSH. 68,999/- | TSH. 108,999/- | TSH. 85,999/- | TSH. 104,999/- | TSH. 69,999/- |
| (VAT IMEJUMLISHWA) | (VAT IMEJUMLISHWA) | (VAT IMEJUMLISHWA) | (VAT IMEJUMLISHWA) | (VAT IMEJUMLISHWA) | (VAT IMEJUMLISHWA) |

**POCHI KWA WATEJA 500 WAKWANZA BURE**

## ZINAPATIKANA KATIKA MADUKA YA VODACOM YAFUATAYO

***Dar es Salaam*** *- Mtaa wa Ohio 0744 710 220-3, Royal Palm 0744 710 609, Slipway 0744 710 229 •* ***Arusha*** *- Barabara ya Uhuru 0744 710 187*

***Mbeya*** *- Mtaa wa Pasta 0744 710 226 •* ***Moshi*** *- Barabara ya Double 0744 710 189 •* ***Mwanza*** *- Barabara ya Pasta 0744 710 190 •* ***Zanzibar*** *- Mtaa wa Darajani 0744 710 339*

**Ofa ni wakati bidhaa zipo*

**KIFUNGU B**

# TIMU NNE KUTETEA AFRIKA

*Na Stephen Ongaro na Mashirika*

❶ Timu nne- Misri, Cameroon, Nigeria, na Sierra Leone ambazo zilichaguliwa na na Shirikisho la kandanda la Afrika (CAF) mwishoni mwa mwaka jana, ziliwakilisha Afrika katika mechi za kugombea kombe la Meridian la Wachezaji wasiozidi miaka 17, mapema mwaka huu.

❷ Wakilishi wa Afrika walicheza na Ufaransa, Ureno, Uhispania, na Uturuki katika mashindano yaliyofanyika kuanzia Februari 4, 2005 mjini Ankara, Uturuki. Mashindano haya yalipangwa kusaidia Afrika katika kujiendeleza kimchezo katika ngazi za kimataifa.

❸ Tunisia, ambayo mapema mwaka huu iliandaa fainali za Kombe la Afrika na kuibuka mshindi katika fainali ilipoishinda Morocco, ilicheza na Uturuki mechi ya kujipima nguvu Februari 9, 2005 mjini Ankara. Mechi hiyo ilikuwa ya kujenga uhusiano kati ya CAF na Muungano wa Kandanda wa Bara la Ulaya.

❹ Mechi nyingine iliyopangwa na CAF ilikuwa mechi kati ya Tunisia na Japan ambayo ni bingwa wa Kombe la Washindi bara la Asia. Tunisia na Japan ziligombea Afro-Asian Nations Cup ambalo lilichezwa mara ya mwisho miaka minne iliyopita.

❺ Sababu iliyofanya shindano kati ya bingwa Afrika na bara Asia kutofanyika ni matokeo ya kura za kuchagua Ujerumani kuandaa fainali za Kombe la dunia za 2006. Wakati wa upigaji kura mwaka 2000 jijini Zurich, Uswisi, wajumbe kutoka bara la Asia walipigia Ujerumani kura na kuinyima Afrika nafasi ya kuandaa fainali za 2006.

❻ Ujerumani ilishinda kwa kura 12-11 dhidi ya Afrika Kusini. Hata hivyo, kwenye upigaji wa kura mwaka huu, Afrika Kusini ilipata nafasi kubwa na kushinda mataifa mengine ya Afrika yaliyojitokeza kuandaa fainali za 2010. Hii itakuwa mara ya kwanza kwa fainali za kombe la Dunia kuandaliwa Afrika tangu kombe hili lianzishwe mwaka 1930.

❼ Kwenye mashindano hayo Afrika iliwakilishwa na timu tano. Kampeni za timu za Afrika kuwania nafasi hizo tano zilianza mwaka jana na kuendelea mapema mwaka huu. Timu 30 za Afrika ziligawanywa katika makundi matano ya timu sita. Mshindi kutoka kila kundi alifuzu kwa fainali. Timu mbili bora kutoka kila kundi zilifuzu kwa fainali za Kombe la Afrika za 2006 nchini Misri. Timu 10 ambazo zilifanya vyema zilikuwa na uhakika wa kwenda Misri.



❽ Nafasi nyingine tano zilitengewa timu ambazo zilifanya vyema kwenye makundi yao wakati wa mechi za mchujo. Ghana itakuwa mwandalizi wa fainali za 2008.

**KIFUNGU C**

# KWA NINI WANAWAKE WENGI HAWAKOSI MKOBA?

Ni kifaa pekee ambacho ni wanawake wachache wanaodiriki kuondoka nyumbani bila kuwa nacho. Ukweli ni kwamba thuluthi mbili za wanawake wanakiri kwamba kamwe huwa hawaondoki nyumbani bila kuwa na mkoba wao mkononi. Ikiwa imesheheni vipodozi, pochi, simu ya mkononi, funguo na shajara, mikoba imekuwa kama silaha kinga kwa wanawake na huwawezesha kukabiliana na kitu chochote kinachoweza kujitokeza kutwa nzima. Na kwa mujibu wa utafiti, mkoba aubebao mwanamke huwa ni ishara muhimu kuhusu haiba yake.

Aina ya kwanza ni ile ya mwanamke ambaye ni mwangalifu kupindukia. Huyu hupendelea mkoba unaofaa kimatumizi na wenye mpangilio mzuri. Nusu ya wanawake barani Afrika huingia katika kundi hili la wanawake wasiokuwa na masihara. Kwa mujibu wa uchunguzi uliowashirikisha wanawake wapatao 2,000 kutoka nchini Kenya na Tanzania, wanawake waliobaki wanaingia katika makundi mengine manne.

Mwanamke mmoja kati ya 10 huangukia katika kundi la mateka wa fasheni. Kundi hili lina tabia ya kuwaiga wanawake maarufu na hupendelea mikoba yenye rajamu zinazovutia sana. Mfano mzuri wa kundi hili ni Orie Rogo Manduli. Orie Rogo Manduli huwa haachani asilani na mkoba wake wenye rajamu ya Louis Vuitton.

Asilimia 11.3 ya wanawake walioshirikishwa katika uchunguzi waliainishwa kama watu wenye tabia ya kugandana na mazoea. Hawa huendelea kutumia aina ile ile ya mkoba kwa muda mrefu sana. Maisha yao yanatawaliwa na desturi na mazoea. Mfano mzuri wa kundi hili ni Mama Ngina Kenyatta ambaye huwa haachani asilani na mkoba wake mweusi.



Mwanamke mmoja kati ya wanawake 10 huangukia katika kundi la wasichana wenye vurugu. Hawa hupendelea mikoba mikubwa mikubwa ambamo hushindilia vitu mbalimbali, jambo ambalo huashiria maisha yao yaliyojaa vurumai. Wanawake katika kundi hili hubeba mikoba ya ajabu ajabu.

Aidha kuna kundi la waumini wa fasheni ambao hupenda kubadili mkoba kwa kila tukio. Uchunguzi huu uligundua kuwa zaidi ya mwanamke mmoja kati ya wanawake watatu walio na uwezo hununua mkoba kila baada ya miezi miwili.

**KIFUNGU D**

# MADHARA YA ULEVI

Kuna majadiliano makali yanayoendelea kuhusu faida za ulevi au madhara yanayofungamana na tabia hii, hasa ikiwa imepindukia kiasi. Baadhi ya watu hudai kuwa tembo kidogo ni zuri kwa afya, humletea mtu uchangamfu, hufanya watu waweze kujumuika pamoja, ni sehemu muhimu ya burudani hivyo wale wanaoshiriki huitumia kama njia ya kujipumzisha kutokana na kazi nyingi za mchana.

Kuna mawazo mengine kuwa manufaa yanayopatikana katika unywaji pombe ni machache ilhali madhara yanayopatikana ni mengi. Watu hawa wanadai kuwa: afya ya mwenye kutumia pombe huharibika kupindukia, jamii nyingi huachwa katika hali ya mateso, watoto mara nyingi huharibiwa maisha yao na wazazi wanaodumu katika ulevi, ulevi husababisha vifo, husababisha ajali za barabarani, huleta umaskini katika familia hasa ikiwa pato lao ni ndogo, husababisha ugomvi na vita katika jamii, saa nyingi katika kazi huweza kupotea na maendeleo ya nchi kwa jumla huzorota.

Katika nchi nyingi duniani, kuzuia tu tembo hivi hakuwezekani. Maelfu kwa maelefu ya watu wameajiriwa katika viwanda vya tembo. Hata hapa Afrika ya Mashariki biashara ya pombe ni sehemu ndogo lakini muhimu kiuchumi. Kuweka vikwazo juu ya pombe si kuingilia sehemu moja ya uchumi tu, bali pia ni kuingilia maisha ya watu binafsi. Basi je, tuwaache baadhi ya watu waendelee na tabia ambayo inawadhuru wao na wengineo? Tabia ya binadamu huweza kunyosheka kwa njia mbili: kwa mawaidha mema au kwa kanuni za kisheria. Basi kwa nini njia zote mbili hazitumiwi katika kukomesha ulevi? Jambo hili limesababisha baadhi ya walevi wa afyuni na bangi kuuliza kwa nini watu huadhibiwa na sheria wanapotumia ulevi wa bangi na afyuni lakini huachiliwa huru wanapotumia ulevi wa pombe? Je, hivi si kuonyesha kuwa sheria inabagua juu ya namna mbili za ulevi zinazowadhuru watu?



Ili kupunguza ulevi hasa ulevi uliopindukia serikali inaweza kufanya mambo yafuatayo: kuelimisha watu katika jamii, shuleni na vyuoni juu ya madhara ya ulevi, kutia kanuni za kisheria kwa wale wanaoshiriki katika ulevi, kutenga kiwango cha pombe ambacho mtu hastahili kupitisha, kushirikiana na kampuni zinazotengeneza pombe juu ya njia bora za kutumia pombe bila kuidhuru jamii na maendeleo kwa jumla.